UFUPISHO WA ALIFU LELA ULELA KITABU CHA KWANZA

Posti hii inakwenda kukisimulia kuhusu hadithi za alifu lela ulela KITABU CHA KWANZA

UFUPISHO WA ALIFU LELA ULELA KITABU CHA KWANZA

Katika nchi za China, Hindi, Uarabuni na Uajemi alikuwepo mfalme aliyefahamika na kuheshimika sana kwa uhodari wake na utawala wake mzuru. Mfalme huyu alikuwa na watoro wawili ambao ni Shahariyar na Shahzaman. Watoto hawa walikuwa mahodari na walifahamika sana. Alipofariki baba yao mtoto mkubwa alitawala kiti cha baba yake kuanzia makao makuu na mdogo wake akaendelea kutawala maeneo ya Samarqand.

Baada ya kutengena kwa muda ndugu wawili hawa walipanga kukutana. Makutano yao yalifanikiwa kupangwa na hatimaye wakakutana. Katika wakati kama huu wa kukutana kwa ndugu wawili hawa kulitokea hali za kusalitiwa na wakezao. Shahariyar alikuwa na mkewake aliyempenda sana na hakuamini kuwa inaweza kutokea siku akasalitiwa na mkewe. Baada ya usaliti huu aliamini kuwa hakuna tena mwanamke mkweli duniani kote. Hivyo akaweka nadhiri ya kuoa mke mpya aliye kigori na kumuuwa kila ifikapo asubuhi.

Kiapo hiki cha Sultani huyu kilikuwa kweli na alikuwa akifanya hivyo yaani anaowa jioni na asubuhi anauwa. Hali ilikuwa ngumu kiasi kwamba watu wakawa wanawakimbiza mabinti zao mjini. Sifa zote nzuri za Sultani huyu zikaanza kuwa mbaya kwa kitendo chake cha kuuwa watoto wa kike. Kazi yote ya kutafuta mabinti wa kuolewa na mfalme pamoja na kazi ya kutekeleza ahadi ya mfalme kuwauwa mabinti hawa alipewa mmoja katika mawaziri wa Sultani huyu.

Sultani huyu alikuwa na mabinti wawili ambao ni Schehrazade na Dinarzade. Mabinti hawa walikuwa ni wazuri sana na walipendana na hata hivyo walipata upendo mkubwa sana kutoka kwa mbaba yao. Schehrazade ambaye ndiye mkubwa alikuwa ni mrembo zaidi na alikuwa na taaluma mbalimbali na alikuwa na elimu za mambo mengi hata ya kisayanzi na masimulizi ya fasihi. Watu wa nchi hii waliamini kuwa uzuri alonao Schehrazade anafaa kuilewa na mfalme au mtoto wa mfalne na si mtu mwingine.

Sikumoja katika mazungumzo ya kifamilia kati ya waziri na watoto wake Schehrezade alitowa ombi la kushangaza kwa baba yake na kumwambia kuwa anatakakukomesha tabia ya mfalme ya kuuwa mabinti hivyo anataka siku ifiataya aolewe yeye. Waziri alishangaa na kumuonya mwanae lakini hakusikia. Akajaribu kumtisha na akamsimulia hadithi ya mfugaji na mkewe lakini msmamo wake hauku badilika. Basi harusi ikafanyika na Shehrazadw akapanga mpago na Dinarzade juu ya kutaka kukomesha tabia ya Sultani.

Usiku nyumbani kwa mfalme Dinarzade alisikika akimuamsha dadayake Schehrazade ambaye anatarajiwa kuuliwa ifikap asubuhi. Dinarzade alimwambia dada yake apigie hadithi nzuri iwe kama ndio mazungumzo ya kuagana. Schehrazade aluimtaka idhini mfalme na kukubaliwa. Akaanza kumsimulia hadithi ya mfanya biashara na jini. Masimulizi ya hadithi hii yalionekana kumvutia na Sultani pia. Schehrazade kwa ufundi wake wa kusimulia hadithi aliikata hadithi hii na kumwambia Sultani akimuongeza siku zaidi ya kuishi ataimaliza.

Sultani alimpa siku zaidi Schehrazade ili amalizie hadithi zake. Utamu uliendelea kumpanda Sultani na kila siku hadithi zilikuwa zinaishia patamu. Hivyo Schehrazade akaendelea kupata muda zaidi wa kuishi. Dada huyu alisimulia hadithi ya mvuvi na jini, hadithi ya chongo watatu na mabinti wa baghadad na nyinginezo hata akafikia kwenye hadithi ya Sinbad. Dada huyu alipomaliza hadithi hii akabakiwa na kuelezea yalotokea kwa mtoto wa Sinbad.

Basi siku ilofata baada ya kuisha kwa hadithi ya Sinbad Scheherazade akaanza kusimulia kilichotokea kwa mtoto wa Sinbad alozaliwa na bint ‘Aisha mtoto wa mfalme. Scheherazade akamueleza kuwa atahaya ya msimulia hadithi nzuri zaidi ya ile a mtoto wa Sinbad. Hapo Sulltani akamwambia asimulie hiyo hadithi nzuri zaidi ya mtoto wa Sinbad. Hapo Scheherazade akaanza kusimulia hadithi ifuatayo.

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Kifo cha mtoa burudani wa sultani

Posti hii inakwenda kukusimulia kuhusu hadithi ya kifo cha mtoa burudani wa sultan

KIFO CHA MTOA BURUDANI WA SULTAN.

Hapo zamani katika mi wa Baghadani wakati wa utawala wa Sultani Harun Rashid alikuwepo kijana mmoja aliyekuwa karibu sana na Sultani kwa kuwa alikuwa akimpa burudani. Kijana huyu alizoeleka sana na mfalme kiasi kwamba mfalme hakuwea kumkosa hata kwa siku moja. Siku moja kijana huyu akiwa kwenye dimbwi kubwa la mawazo alitembea maeneo kadhaa katika mji huu na akakutana na Mshona nguo. Alikaa sana kwenye eneo hili nje ya ofisi ya mshona nguo.

Muda wa kufunga ofisi ulipofika mshonanguo alimchukuwa kijana huyu na kwenda naye nyumbani

kwa lengo la kufurahi nae na kula chakula. Alipofika nyumbani mkewake alimpokea kwa ukarimu kijana huya. Na kwa ufundi na uwezo wa kutoa burudani alio nao kijana huyu aliweza kuchangamsha nyumba hii. Mke wa mshonaji alianza kuandaa chakula kizuri sana na nyama ya samaki. Aliandaa ndizi na vyakula vizurivizuri kwa ajili ya mgeni wao.

Huku burudani zikiendelea mke wa mshonaji aliendelea kupika. Mshonaji alikwenda kuchukuwa vinywaji kadhaa na kuvileta pale nyumbani kwao. Muda wa chakula ulipofika walikusanyika na kuanza kula. Katika kufanya manyonjo na furaha mke wa mshonaji akachukuwa nofu la nyama na kuliiweka kwenye mdomo wa kijana yule na kumwambia meza. Kijana alimeza na kwa bahati mbaya kwenye nofu lile kulikuwa na mwiba mkubwa sana. Mwiba ule ukamkaba kijana yule na kupoteza maifahamu.

Mshonaji baada ya kuangalia hali ile akagunduwa kuwa kijana amekufa. Kuona hivyo akaogopa sana maana ataambiwa amemuuwa kijana wa watu. Wakashauriana na mkewake nini wafanye. Baada ya muda wakaamuwa kumchukuwa marehemu waendenae kwa tabibu ili wamuachie msala wote tabibu. Hali ikawa hivyo na wakambeba hadi mlangoni kwa tabibu kisha wakamlaza pale.

Waligonga hodi akatoka kijana wakamueleza amuite abibu harakwa kuna mgonjwa ana hali mbaya. Alipoingia ndani yule mtto kwenda muita tabibu mshonaji na mkewe wakakimbia. Tabibu alitoka na kiza cha usiku ule na akamkanyaga huyo aloambiwa mgonjwa. Ikawa tabibu akafikiri yeye ndo alomuuwa mgonjwa. Akanza kushauriana na familia yake wajue namna ya kujinusuru na janga lile. Mke wake akamshauri mumewe kwa kumwambia kuwa wamueke kwenye ukuta wa jirani yao.

Jirani yao alikuwa ni muuza nyama hivyo kulikuwa na wezi wanakuja kuiba nyamma pale kwake. Hivyo walifikiria huenda akampiga na kujuwa amemuuwa yeye. Basi wakamfunga kamba karehemu yule na kumpenyeza kwa nje ya nyumba yao kupitia paani. Aliposimama sawa kwenye ukuta wa jirani yao kwa nyuma wakaitowa kamba ile. Ilipofika usiku sana yule muuza nyama alirudi nyumbani na alipoona mtu kasimama kwenye ukuta wake akajuwa ni mwizi amekuja. Hivyo akachukuwa fimbo kubwa na kuanza kumtandika sawasawa. Hatimaye mtu yule alianguka na alipomgusa akahisi ameshakufa.

Kwa woga akafikkiria kuwa ameuwa mtu. Akaanza kushauriana na familia yake namna ya kujinusuru na mkasa huu.wakaamuwa wambebe maiti yule kisha wakamsimamishe kwenye moja ya kuta za sokoni, huenda akakumbana na walinzi wakampiga na hapo itakuwa ameuliwa mwizi na esi itaishia hapo. Wakafanya hivyo na baada ya muda mmoja katika walevi akapita eneo lile na alipoona mtu kajibanza akajuwa ni wale watu wanaomnyemelea siku zote na kumuibia pindi akilewa.

Mlevi yule alinyata pale karibu na kumpiga chupa ya mgongoni mtu yule. Hatiumaye kwa pigo moja la mlevi mtu yule akaangunga na m;evi kuangalia vile akajuwa kuwa ameuwa. Palepale walinzi walifika na kumkamata mlevi yule kwa kosa la kuuwa mtu. Basi kesi ile ikapelekwa kwa kadhi ili hukumu itolewe, na hukumu ikapita kuwa mlevi ni muuwaji hivyo naye auliwe. Mlevia akapelekwa katika uwanja wa mauaji na kuwekwa tayari kuuliwa.

Wakati hukumu inataka kupitishwa ghafla akatokea yule muuza nyama na kusema “ewe ndugu hakimu tafadhali niuwe mimi kwani ndiye nilomuuwa huyo kijana na si huyo mlevi” basi pale pale akaondolewa mlevi na muuza nyama akatiwa kitanzi tayari kwa kuchinjwa. Kabla hajachinjwa akatokea tabitu na kusema yeye ndiye muuwaji hivyo achinjwe yeye. Na alipotaka kuchinjwa tabibu alikuja mshona charahani na kusema yeye ndiye muuwaji halisi na wote hawa hawahusiki. Kitanzi kilipokuwa kwa mshona charahani. Kabla ya kufanya zoezi hakimu akaanza kushauriana na wenzie nini wafanye maana muuwaji halisi hawamjui.

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Nani muuaji?

Posti hii inakwenda kukusimulia kuhusu muuaji wa mtoa burudani wa sultan

NANI MUUWAJI?

Mfalme alipoamka alitaka kumuona kijana wake lakini asimuone. Akauliza habari za kijana yule na akaelezwa kuwa amefariki lakini muuwaji hajulikani, mpaka sasa kuna wauwaji wanne na kila mmoja anadai yeye ndio muuwaji halisi. Mfalme akaamrisha wote waitwe na waje mbele yake na amtafute muuwaji halisi wa kijana wake yeye mwenyewe.

Mfalme aliogopa sana asije fanya kosa kama lile alolifanya kwenye kesi ya kifo cha mtoto kwenye ndoo ya maji ambapo mtu asiye na hatia aliuliwa. Walinzi wa mfalme wakamuuliza kwani ni kitu gani kilitokea kuhusu kesi ya mtoto huyu. Akawasimulia kwa ufupi habari hii kuwa alikiwepo mama mmoja aliyekuwa na mtoto anayeanza kusimama dede. Pale ndani palikuwepo na mfanya kazi wao. Mtoto yule alizoeshwa kuogeshwa kwenye ndoo ya maji na mama yake a alikuwa akifurahia sana anapotiwa kwenye ndoo ya maji.

Siku moja mama yule alipata safari ya ghafla na kumuacha mtoto wake kwa jirani maana mfanyakazi hakuwepo alikwenda kuchota maji mbali kidogo. Mtoto yule akiwa kwa jirani alitoroka na kyurudi kwao. Na kwa kuwa milango ilikuwa wazi aliingia ndani na kukuta ndoo za maji zipo wazi. Mtoto yule akaingia kwenye ndoo zile na kupitiwa na usingizi. Dada mchota maji alipokuja hakuangalia vizuri kwenye ndoo akajaza maji na kuondoka kwa haraka ili akawahi foleni ya maji.

Mtoto mule kwenye ndoo alipiga kelele na kayanywa maji zaidi na hatimaye akapoteza maisha. Akaja dada wa kazi na kujaza ndoo ile kisha akaifung bila ya kuangalia nddani. Akazipandanisha ndoo kama tatu. Mama aliporudi alimtafuta mtoto kwa jirani bila ya mafanikio. Juhudi za kumtafuta ziliendelea ndani ya siku tatu bila hata kufanikiwa. Majirani wakamuonea huruma mwenzao na wakaamua kumpikia apate kula, wengine wakaanza kufua nguo zake na kudeki nyumba maana ndani ya siku tatu hakukuwa kukipikwa wala kufagiliwa wala kudekiwa.

Maji yalipobakia ndoo moja wakamkuta mtoto amshakufa kwenye maji. Mama yule kwa hasira alimpeleka mfanyakazi wa hakimu na hatimaye mfanyakazi akauliwa kwa kosa la kumuuwa mtoto kwenye maji na kumficha na ndoo. Kumbe mfanya kazi hana hatia maana ni mama aliyemzoesha mwanae kuingia kwenye ndoo na nikosa la jirani kutomuangalia vizuri mtoto. Kosa la mfanyakazi kuweka maji bila ya uangalifu. Hivyo nahofia kesi hii isijekuwa na mfanano na hii. Basi kwa haraka akaagiza waletwe wat wote wanaohusika mbele yake.

Watu wote wakapelekwa kwa mfalme pamoja na maiti wao. Falme akaanza kuuliza mmoja mmoja ataje amemuuwa vipi. Hapo mlevi akasema namna ambavyo tukio limetokea, kisha muuza nyama akaeleza tukio lilivyotokea kwa upande wake kisha tabibu kisha mshona nguo. Baada ya kiusikia maelezo ya kushangaza mfalme akaamuru habari hii iandikwe kwa wino wa dhahabu na iwekwe kwenye kumbukumbu za kifalme. Kisaha mfalme akauliza je kuna mwenye hadithi inayoshangaza zaidi ya hii ya kijana wangu huyu? Hapo mlevi akasema yeye ana hadithi ya kushangaza zaidi ya hii. Na akaanza kusimulia kama ifuatavyo;-

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Hadithi iliyosimuliwq na mlevi mbele ya sultani

Posti hii inakwenda kukusimulia hadithi iliyosimuliwa na mlevi mbele ya sultan

HADITHI ILIYOSIMULIWA NA MLEVI MBELE YA SULTANI

Tambua ewe Sultani muadilifu wa Baghdad mwa na wa Rashidi utambulikae kwa Harun, tambua kuwa mimi ni mzaliwa wa Misri na huku nimefika tu kwa sababu za utafutaji wa riziki. Baba yangu alikuwa ni mfanyabishara mzkubwa sana huko misri. Alijulikana sana katika miji na hata viji na nchi za majirani ya misri. Nilikuwa nikishiriki biashara na baba yangu toka nilipokuwa mdogo.

Hatimaye Mwenyezi Mungu akamchukuwa baba yangu na hapo mimi nikarithi kazi ya baba. Katika familia nipo peke yangu na mama yangu alishafariki zamani sana nikiwa mdogo. Nilifanyabiashara misri. Biashara yangu kuu ilikuwa ni kuuza kanzu. Nilikuwa nikizipaka manukato mazuri hata zikawa zikinukia sana na kumvutia mpita njia.

Watu walipenda sana biashara yangu na jina langu lilikuwa hata kumzidi baba yangu. Ila katu sikuweza kusafiri kibiashara kama alivyokuwa akifanya baba yangu. Niliweza kutengeneza chaneli za kibiashara wakawa wafanyabiashara wadogowadogo wanachukuwa mzugo kutoka kwangu. Kwa hakika biashara ya kanzu ilikuwa ikinilipa vyema. Kipindi chote hiki sikuwa mwenye kuoa.

Ilitokea siku moja akaja mtu mmoja na kuulizia bei ya kanzu. Badala ya kumtajia akanipatia kiasi kikubwa cha fedha na kunieleza nimpelekee mzigo wake sehemu ambayo alinitajia. Haikuwa ni kazi nzito kwani ni katika majukumu ya kazi yangu. Nilipomaliza maandalizi nikampelekea mzigo wake. Alipouona akanieleza kuwa nimuuzie mzigo ule pale kwake na faida yeyote nitakayoipata tutagawana.

Kwa uchu wangu wa pesa nikakubali. Yule bwana akaniaga safari ila akanieleza nimtunzie pesa yake mpaka atakapo rejea. Mambo yakawa hivyo nilimaliza kuuza mzigo na nilipata faida kubwa sana. Yule bwana baada ya mwezi akaja na kuniulizia pesa yake. Nikamueleza kuwa ipo salama. Basi akanieleza nimtunzie hadi atakaporudi tena.

Baada ya mwezi akarejea, na kuniambia kuwa ana shughuli nyingi, baada ya kumaliza atakuja kuchuuwa pesa yake. Alipoondoka akakaa kiasi cha mwezi. Hata aliporudi alikuwa mapendeza sana. Alifaa nguo nadhifu na za kupendeza.. alipokuja akanieleza ataondoka tena ila akirudi atachukuwa pesa yake. Mimi nikajiapiza kuwa pindi akija nitamkirimu kama mgeni wa heshma.

Safari hii alikaa kama mwaka hivi na aliporudi akaulizia pesa yake nikamueleza kuwa ipo salama. Basi nikamuomba awe mgeni wangu kwa siku ile na akakubali kwa sharti kuwa matumizi nitakayotumia yasiwe katika ile pesa yake. Nikakubali, baada ya muda kikaletwa chakula safi sana. Nikamnawisha kisha akanawa mgono wa kushoto. Nilistaajabu sana. Apilpoanza kula akala kwa mkono wa kushoto.

Nilistaajabu sana kwa mtu mtanashati na msafi kama huyu alafua anakula kwa shoto. Tulipomaliza kula akanywa maji kw ashoto. Basi baada ya chakula tukaanza kuzimulia za hapa na pale. Ndipo nikamuulza anitoe mashaka kuhusu kula kwake kwa shoto. Huenda ana ugonjwa ama ameumia ama anafanya masifa. Ndipo akatoa mkono wake. Looo! Mkoni wake ni kugupu aani ni kiwete ana mkono lakini kiganja kimekatwa.

Baada ya hapo akanieleza kuwa si kama ametaka kula na kushoto ila kuna sababu ilopelekea hali hiyo. Basi kwa udadisi niauiza kuhusu chanzo bila kusita ndipo akaanza kuzimulia hadithi yake na kukatwa kwa mkono wae:-

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Hadithi ya kilema, mtanashati asiye na mkono

Posti hii inakwenda kukuletea hadithi ya kilema, mtanashati asiye na mkono

HADITHI YA KILEMA, MTANASHATI ASIYE NA MKONO

Basi tambu kuwa mimi ni Mtu wa Baghadad na ni mtoto wa aliyekuwa mfanyabishara mkubwa sana. Nilipokuwa mdogo nilisikia wafanyabiashara wakitoa sifa kemkem kuhusu miji ya misri na uzuri wake. Walikuwa wakisifia jinsi mto Nile unavyokwenda kwa kasi na kupendezesha macho. Majumba makubwa ya wafalme na mafarao wa Misri. Hawakuacha kusifia uzuri wa masoko na mabinti wa Misri.

Basi wakati alipofariki baba yangu mimi nikawa ndiye msimamizi wa mali zake. Katika familia yetu nilikuwa peke yangu yaani sikuwa na mama wa la baba na nilizaliwa peke yangu. Basi niliendelea kukuza biashara aliyoiacha baba yangu. Na ilikuwa ni kuuza kanzu pamoja na nguo za kike. Nilikuwa nikiuza vitamaa vya kujifunika kwa wanawake ambavyo vimechovywa na dhahabu

pamoja na kuwekewa harirriri.

Watu walipenda sana aina za mavazi nilizokuwa nikiuza.nilibahatika kupata wateja wa jumala na rejareja. Sifa za nguo zangu zilienea bara la arabu hata zikafika Misri. Niliweza kupata wateja wa kike na kiume. Niliongeza ujuzi wa kuchovya nguo zangu na marashi pamoja na mafuta ya miski. Kwa hakika hazikuisha kunukia katu.

Sikumoja walipata kunijia wafanyabiashara wa kutokea misri. Walikuwa wakitoa sifa nyingi sana. Hata nikavutiwa na mimi kwenda Misri. Nikaanza kuwauliza maswali kuhusu bidhaa na naman aya soo lilivyo. Nikaandaa bidhaa zangu na kujiandaa kwa safari kuelekea Misri. Baada ya maandalizi kukamilika nikatoka na Ngamia wangu tulipia maeneo mbalimbali yakiyo ya kuvutia. Tulivuka bahari ya na kuingia Misri. Nikatafuta nyumba ya wageni na kulala nikiwa mimi na wafanyakazi wangu.

Ilipoofika asubuhi nikaanza kuchunguza mjini vyema na kutafuta eneo salama kwa biashara. Katika pirika nikakutana na meya wa Mji na kumuelezea shida yangu. Hapo akanielekeza kwa wafanyabishara wadogo. Basi nikaingia mkataba na wafanyabishara wadogo kwa makubaliano kuwa watauza bishaa zangu kisha nitakuwa ninkikusanya mapato kila siku ya alhamisi. Pia nitakuwa nikiwalipa kulingana na faida kwa kiasi maalumu. Wafanya bishara wengi wa Misri huwa wanatumia njia hii.

Basi nikawa kila alhamisi nakwenda kufuatailia mapato yangu na kisha ninawapatia ujira wao. Nikawa naagiza bidhaa kwa jumla kutokea maeneo mbalimbali kisha ninawapatia wauzaji. Kwa hakika Misri kulikuwa kukinipatia faida kuliko Baghadad. Nilifanya hivi kwa muda wa miezi 2 na nusu.

Sikumoja nilikaa dukani kwa wauzaji wangu nikiwa ninakunywa tangawizi iliyotokea china. Akaja msichana mmoja wa makamo kati ya miaka 21 mpaka 25. alikuwa amefunika sura yake, kama ilivyo tamaduni kwa waislamu. Kwa muonekana anaonekana ni msichana kutoka familia ya kitajiri. Basi alisogea mpaka pale nilipokaa na akakaa pembeni yangu. Hapo ndipo nilipopata kusikia sauti yake na harufu ya manukato yake. Hakika sijapatapo kupata harufu nzuri kama ile. Kwa muda huo aliweza kuteka fikra zangu na moyo wangu hata nisiweze kuhisi ladha ya tangawizi niliokuwa nikinywa.

Nilibakia mdomo waki nikiwa na maswali mengi, huyu ni nani, anataka nini hapa, ni mafuta gani

amepaka, ni kwa nini amekuja kukaa karibu na mimi. Mmmmhhh sikutaka kumuuliza kwa kuhofia kuondoka kwake. Baada ya muda akaanza kuulizia bei za vitambaa vya ushungi, ambao una michirizi ya dhahabu nyekundu na mapambo ya hariri. Aliagizia vitu vya thamani sana hata nikafikiri atakuwa ni mtoto wa Mfalme.

Baada ya kuagiza akataka aruhusiwe achukuwe bidhaa kisha pesa atamuagiza mtu ailete. Yule muuzaji akakataa na kumueleza kuwa hawezi kufanya hivyo maana leo mmiliki wa bishara yupo. Nilipata kuyasikia vyema mazungumzo hayo. Yule binti alikasirika na kurudisha bidhaa zile na akasema “kwa hakika biashara yako haijali hadhi za watu”. maneno yale yalinichoma sana.

Basi kwa sauti ya upole nikamuita na kumwambia chukuwa hiyo bidhaa uliyoitaka kwani mimi ndiye mmiliki. Ukipenda utarudisha pesa usipopenda pia itakuwa ni sadaka yangu kwako. Maneno haya niliyasema bila ya kufikiri gharama ya bidhaa zile. Yule bint alinisogelea na kunieleza “Mungu akubariki kwa hisani yako, Naomba akupe afya njema ujekuwa mume wangu”. maneno haya yalikuwa ni kama msumari wa mshangao uliokita kwenye moyo wangu.

Nikamsogelea zaidi ni kumwambia ningepata japo kuona sura yako. Basi akasogea zaidi na kufunua kidogo kitambaa kilichoziba sura yake. Nilibaki kukodoa mimacho, hakika sijapatapo kuona uzuri huo kwa mwanadamu. Macho ya kuvutia yaliyozungukwa na nyusi nzuri zilizo nyeusi sana. Ngozi iliyo laini iliyokaa vyema kwenye shavu la binti huyo. Kwa haraka binti alishusha kitambaa na kupotelea njiani.

Sikumuuliza jina lake na hata wapi anakaa. Nilijuta sana maana nilitamani niwe ninamuona kila muda, kila saa, kila wakati. Nikamuuliza muuzaji wangu kuhusu taarifa za binti yule, naye hakuwa akifahamu jambo lolote. Siku hiyo sikupata hata lepe la usingizi, maana sura ya binti ilikuwa ikinijia usiku kucha. Nilitambua kuwa moyo wangu amekwenda nao wote.

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Binti huyu Ni Nani?

Posti hii inakwenda kukuendelezea hadithi kuhusu kifo cha mtoa burudani wa sultan

BINTI HUYU NI NANI?

Siku iliyofuata nilioga mapema, kisha nikavaa ngu zangu safi na kuelekea pale dukani. Loo! Yule binti akaja tena, alipokuja moja kwa moja akakaa karibu nami na kutoa kitambaa kilichofungwa bundu. Kisha akaniambia " Chukuwa hii malipo yako kwa bidhaa yako siku ya jana". nikachukuwa na kumpatia muuzaji wangu ahifadhi. Sikuwa na haja ya kuhakiki kama pesa imetimia ama laa.

Basi nikaendelea kuzungumza naye maneno ya hapa na pale. Kisha nikaanza kuchomekea maneno ya ishara. Bila shaka alizifahamu vyema ishara zangu. Kwa ghafla alionyesha kukasirika na ndipo alisimama na kuondoka zake. Nilijijutia nafsi yangu kwa nini nimeongea naye kwa ishara za mapenzi. Aliondoka tena bila hata kuniambia anaitwa nani na wapi anakaa. Aluondoka hata sijazungumza hasa nini kipo moyoni kwangu.

Hakika siku hiyo niliiona ndefu sana na sikuweza kula chochote. Nilipata pia kujiwazia huenda binti yule sio mtu wa kawaida, huenda ni jini ama malaika ametumwa kuja kunijaribu. Siku ya tatu yake nikaamua kutembea mjini nkiamini huenda nikakutana naye kwa bahati mbaya. Loo! Sikuiliisha bila hata kukutana na sura yake.

Siku ya nne nilikaa kenye duka lile na ghafla akanijia bibi mmoja. Akanieleza kuwa ameagizwa na bosi wake aje anichukuwe ana mazungumzo. Bibi alikuwa ni mjakazi katika jumba la kitajiri. Nilifahamu hilo baada ya kuona mavazi yake. Nilikubali wito kwa kuamini atakuwa ni yule mrembo aliyeteka hsia zangu, aliyechukuwa moyo wangu, aliyenikosesha hamu ya kula wala kulala.

Niliongozana na bibi yule hata tukafika kwenye nyumba ya wageni. Hap akanieleza niingie kwani bosi wake yumbo ndani. Nilipoingia tu nikakaribishwa na manukato yanayonukia kwa uzuri sana, Loo! Alikuwa ni yule mrembo, alikuwa amependeza sana siku hii. Alvaa mavazi marefu yenye rangi za kuvitia kama tausi. Akanikaribisha kwnye busati lililotandika katikati ya chumba.

Hapo wakaja mabinti wengine wawili vigori, wakaleta vinywaji na kukaa pembeni. Akanieleza kuwa hawa pia ni wafanya kazi wake. Hawezi kukaa peke yake kwani faragha ya mwanaume na mwanamke wasio oana hairuhusiwi kwenye dini. Basi tulianza kuzungumza hapa na pale wakati huo mabinti wale wapo. Mwisho niamueleza uhalizi wa moyo wangu juu yake, ni kiasi gani ninampenda, ni taabu gani nimeipata kwa siku tatu hizi toka niutane naye.

Nilimueleza vyeote kuhusu kuwa sikuwa na usingizi wala sikuona tamu ya chakual. Wakati wote niliokuwa nachungumza yeye alikuwa akitokwa na machozi tuu. Moja wa mabinti wale akachukuwa kitambaa cha hariri kilicho zungushiwa na dhahabu nyekundu, na kutiwa manukato yanayonukia kama miski nyekundu ya kutoka india. Alimfuta machozi kisha akasema " kwa hakika unayoyasema ndiyo yaliyomkuta bosi wetu, toka majuzi anakazi ya kukuwaza, kukutaja, kukufikiria, hali, halali, hanywi kwa upendo alionao kwako".

Nilitamani kumfuta machozi ila nikaogopa kumvunjia heshima mbele ya wafanyakazi wake. Ndipo akasema kuwa " kwa hakika walioyasema ndugu zangu ni sahihi, wewe ni mtu wa kwanza kukupenda, na amini nakupenda kweli, naomba tuoane. Kwani siwezi kukukosa tena, siwezi kuonja tena adhabu ya kuwa mbali nawe, uso wako kama lulu kwangu, katu sichoki kukutazama, tabasamu lako…… mmmhmmh nakupenda sana."

Basi aliendelea kuzungumza kisha tukakubaliana kuwa tuoane ila ndoa iwe kwa siri kwa sababu, mimi ni mtu ambaye bado ni mgeni hivyo haitakuwa vyema kutangaza harusi yetu, na mimi ninatambulikamkwa utajiri nilio nao, hivyo wanaweza kukufanyia fitina, na hata kukuumiza. Siku ilofata ilikuwa ni ijumaa. Basi akanielekeza kwake ili niende baada ya kuswali ijumaa ili ndoa ikafanyike. Basi tukaagana pale na mimi nikaondoka na wao wakaelekea zao.

Sikuwa na haja tena ya kulijuwa jina lake maana niliamini kuwa nitalijuwa siku ya harusi. Nilijuwa kuwa yeye ni tajiri na ni mtoto wa tajiri. Niliamini ili niweze kuishi naye ni lazima nitumie pesa vyema. Basi siku hiyo sikuweza tena kulala kwa kuisubiri asubuhi ifike, ili nikamuoe kipenzi maridhawa.

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Ndoa ya Siri yafanyika

Posti hii inakwenda kukuendelezea hadithi kuhusu kifo cha mtoa burudani wa sultan

NDOA YA SIRI YAFANYIKA

Hatimaye siku ya ijumaa ikafika na mimi nikaoga nyema na kuchukuwa kanzu iliyo nadhifu zaidi. Nikaifaa na kujipaka manukato maridadi na kuwa mtanashati ka kuelekea kwenda sala ya ijumaa.

Mapema nilifika msikitini na kuanza kumuomba Mungu. Kwa furaha nia shauku nilioa nayo hata sikuweza kulala msikitini. Baada ya sala kuisha nilitoka masikitini na tayari kuelekea kwa kipenzi changu mtarajiwa.

Nilichukuw amashahidi wawili kwa siri, na hawa walikuwa ni wafanyabiashra wenzangu wa kutokea Baghadad. Tulipanda magari ya kuburuzwa na farasi. Tukafika katika nyumba niliyoelekezwa na tayari kugonga mlango. Mabinti wawili wengine walio wazuri sana wakafungua malango na sisi watu watatu tukaingia. Tulikutanan na ukumbi mzuri wenye malumalu za almasi. Ukuta uluojengwa vyema na kutiwa mapambo ya madini ya fedha a almasi.

Nikaangalia vyema nikaona mapambo yenye kuchorwa kwa lugha ya kiarabu kilicho pendeza. Tuliweza kusogea kila chumba kikiwa kina mapazia marefu yenye rangi za kupeneza sana. Mapazia yalikuwa na michirizi ya madini ya silva pamoja na mapambo ya nayoning'inia mithili ya lulu zilizohifadhiwa vyema. Niliweza kustaajabishwa na manukato ya vyumba hivi ni mazuri sana sijapatapo kuyaona. Tuliendelea hata yukafika kwenye kumbi moja kubwa sana. Hapo tukakuta kuna watu kadha aa wanaume.

Niliweza kuchunguza vyema ukumbi huu nikagundua umepambwa mapambo mazuri sana. Umechorwa michoro ya vippeo michoro iliweza kutiwa rangi za kijani, manjano na bluu. Hakiak niliweza kumpa sifa sana mchoraji. Katikati ya chumba kulukuwa na kiti kikubwa sana cha miguu sita. Miguu iliyopamba kwa vishikizo vya madini ya shaba, magodoro ya hariri yalikaa byema kwenye kiti hiko kikubwa.

Juu ya kiti mzee mkubwa alikuwa amekaa hapo. Nilimtambuwa umri wake ni kati ya 60 mpaka 70. alikuwa na ndevu nyingi na nyeupe zilizomkaa vyema. Alikuwa na sharubu nyupi na mashrafa yaliyo lala vyema. Ndevu zenye afya njema zilizotiwa hina na kufanana vyema. Mzee alivaa kanzi nadhifu yenye manukato zaidi ya watu wote tulio hudhuria. Basi tukakaribishwa vyema nikaka mimi na wenzangu. Jumla tulikuwa wtatu 9.

Bila ya kupoteza muda yule mzee akanitaja kwajina "Je wewe kijana ndiye Ibrahimu Khalidi wa Baghadad?" nilisita kidogo kujibu huku nikiwaza amelijuaje jina langu, na amejuaje kama natokea Baghadad. "ndiye mimi mzee" basi akaniambia nisogee karibu na ndipo akaniuliza maswali kadhaa na nikamjibu vyema. Basi akaniuliza " Kijana Ibrahimu khalid umekubali kumuoa mwanangu Nurat khan"? " hapo ndipo nilipopata kujuwa jina halisi la binti yule na kumjuwa Baba yake. "Ndio nimekubali kumuoa Nurat Khan…"

Baada ya hapo mbele ya mashahidi ndoa ikafungwa. Mashahidi waliweza kupatiwa dhahabu pishi

tano kila mmoja na wakaruhudiwa kuondoka. Mimi nikapelekwa kwa mke wangu. Kwa hakika nilipatapo kuona mambo mengi na mazuri na ya kustaajabisha. Naomba nisielezee hasa kipengelehiki. Basi tukaelekea nyumba nyingine ambapo ndipo binti anaishi. Huko ni mbali na alipo baba yake. Na tukaendelea kumaliza taratibu za usikuwa harusi mimi na mkewangu (……taa ikazimwa…….).

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Kukatwa mkono na kuurithi utajiri

Posti hii inakwenda kukupa muendelezo kuhusu kifo cha mtoa burudani wa sultani

KUKATWA MKONO NA KURITHI UTAJIRI

Basi niliweza kulala kwa mke wangu siku ile na asubuhi nilimuashia kipande 1000 vya dhahabu na kuondoka kuelekea dukani. Jioni niaenda tena kwa mkewangu nikalala na asubuhi jikamuachia vipande 1000 vya dhahabu na kuondoka. Niliweza kufanya hivi kwa muda hata nikafiisika mali yangu yote ikiisha. Nikiwa sina kitu, huku nikiamini kama nitaenda mikono mikavu nitaingia aibu katika familia ya kitajiri.

Nikiwa na mawazo kama hayo mara nikaona sehemumoja kuna msongamano wa watu. Nikasogea karibu nakukuta kuna watu wanapigana. Katika kusogea zaidi mara bikaona mama mmoja ameweka vipande vingi vya dhahabu kwenye kikapu chake kisha amefunika kwa kanga kuukuu. Basi nikasema leo ninaiba nipate kumliwaza mke wangu. Nilisogea karibu na kuingiza fumba la kwanz ana kutoa vipande kama kumi.

Nikaingiza tena mkono na kupata vipande 5 nikajisemea hivi vinatosha. Wakati nataka kuondoka yule mama akashibuka na kuniona. Hapo akaniitia kuwa ni mwizi na haikupita muda nikawekwa mbaroni. Nilijitetea na ndipo nikapelekwa kwa kadhi. Nikasachiwa na kukutwa na vipande vya dhahabu. Basi kadhi akahukumu nikatwe kiganja cha mkono kwa mujibu wa sheria za kiislamu.

Nilikatwa mkono na kupoteza fahamu. Kuja kushituka nipo sehemu ya mbali nimetupwa. Niliweza kujikongoja hata nikafika kwa mke wangu. Nikaufunga mkono wangu ili asiuone. Niliishia kulala na kumueleza kuwa ninaumwa. Kilipokuja chakula nilikulwa kwa moko wa kushoto. Kitebdo hiki

kilimuuuma sana ndipo akataka kuona nini kipi kwenye mkono wangu wa kulia. Nilimueleza kuwa nina jipu ila hakutaka kuniamini.

Alinifungua na ndipo akaanza kuli sana. Basi nikamueleze akila kilichotokea bila hata kuficha kuwa kwa ajili yake nilikusudia kuiba na nikaiba ila nikakamatwa na kukatwa kiganja cha kulia. Basi alilia sana kisha akasema " kwa ajili yangu umekatwa mkono, ulidhani nimekupenea pesa" basi akaagiza aletewe mashahidi wawili ndipo walipokuwa akawaambia washuhudiie kuwa mali za ke zote ni za kwangu, alioroshesha mali nyingi sana, mashamba na majumba mengi yaliyopo mjini. Alipo maliza kuoroshesha akaweza muhuri wake na hati ile ya makubalian ikapelekwa kwa baba mkwe naye akaikubali.

Kila kitu kilivyokuwa sawa aliwalipa mashaihidi na kisha akanichukuwa mpaka kwenye stoo. Huko nikakuta kuna mamia ya masanduku yaliyojaa dhahabu na fedha nyingi. Sanduku moja lilifumikwa kitambaa cha kijani na kuandikiwa kwa lugha ya kiarabu cha asili. Sikuweza kutambua maana yake. Ndip akanieleza kuwa kumeandikwa "kwa kipenzi changu" akanieleza fungua. Loo! Nilipofungua nilikuta vipande vyote vya dhahavu nilivyompa vipo pale kama vilivyo.

Akanieleza kuwa Mwenyezi Mungu amekurudishia mali yako na kukupa ziada, na kukupa mke mwema. Hapo nilimkumbatia mke wangu na kumbusu katikati ya paji lake. Mmhmmmh….(rahaaa). basi nilianza kuendeleza mali za mkewangu tukiwa pamoja. Tuliweza kuishi mika 10 na kubahatika mtoto mmoja wa kike. Miaka mitatu iliyopita mkewang aliumwa na kufariki.

Hivyo kwa ubize niliyokuwa nao ndipo hata nikashindwa kuchukuwa pesa yangu iliyo kwako. Na hii ndio hadithi yangu ya kukatwa mkono. Usidhani nilikula kwa mkono wa shoto kwa kupenda ama majigambo. Baada ya kijana mtanashati kumaliza kuzimulia kisha chake akanieleza kuwa, je ungependa yuende wote Baghadad kibiashara?. nami nikakubali.

Wiki ilofata ndipo tuakaanza safari ya kuja Baghadad. Tulifanya bishara na muda wa kurudi ulipofika mwenzangu alirudi ila mimi nikamueleza kuwa nitaendelea kuishi hapa. Akanieleza nitakaporudi Misri nimpe taarifa maana binti yake atakuwa amefikia kuolewa, hivyo angependa niwe mkwe wake.

Basi niliweza kuishi hapa Baghadad ni mpaka yakatokea haya yaliyotokea leo. Kijana mlevi aliyvyomaliza kusimulia akamwambia mfalme "Je! Hadithi hii si yenye kustaajabisha kuliko hadithi ya kifo cha mtoa burudani wako?" hapa mfalme akasema hapana bado haijafikia kuweza

kuachiwa huru wauhumiwa wa kesi hii. Hapo mjakazi wa Mfalme akaja mbele na usema, nina hadithi ya yaliyotokea kumuhusu huyu aliyekufa, haya yalitokea jana. Naomba nisimulie kama itakuwa na uzito zaidi ya kisa hiki ninaomba watuhumiwa wawachwe huru. Hapo mjakazi wa mfalme akaanza kusimulia hadithi ifuatayo

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Hadithi iliyosimuliwa na kijakazi wa sultani

Posti hii inakwenda kukupa muendelezo kuhusu kifo cha mtoa burudani wa sultani

HADITHI ILIYOSIMULIWA NA MJAKAZI WA SULTANI

Mtukufu sultani, nakwenda kukusimulia tukio lililotokea leo hii wakati tulipokuwa tunaburudika. Tulikuwa tupo kwenye tafrija moja hivi jana wakati wa jioni kabla ya juwa kuzama. Katik tafrija hiyo tulipata kusikiliza usomaji wa quran kwa sauti nzuri sana hata machozi yakatutoka. Baada ya hapo tukabahatika kusikiliza mashiri. Mshairi maarufu kutokea India alikuwepo, na alighani kwa sauti njema sana.

Baada ya burudani kuisha ndipo tukaletewa chakula kizuri sana. Vyakula vya kuoka, na nyama iliyo kaushwa vizuri ililetwa bele ya hadhara. Vinywaji vilivyo vizuri vikahudhurishwa mbele yetu. Basi tulikaa vikundi vikundi kuzunguruka sahani za vyakula. Katika kundi nililokaa nilikuwa na aliyekuwa na shughuli yake siku ile. Na hapa kitu cha kushangaza ndipo kikatokea.

Katika vyakula vilivyoletwa kulikuwepo na zerbajeh. Hiki ni chakula zilichotengenezwa kwa mchanganyiko wa vyakula kadhaa na matunda. Chakula hiki unapokila harufu yake inaweza kukaa kwa muda wa siku nzima kwenye mikono. Ni chakula kitamu na kipendwacho na watu wa Baghadad. Basi ghafla mwenzetu mmoja alipoona chakula kile akaanza kutetemeka na kutokwa na majasho kana kwamba ameona kitu cha kutisha sana.

Yule bwana hakutaka hata kula chakula kile. Sikuwa na wasiwasi sana nikajuwa lamda hali chakula kile, ama lamda kuna mtu anamdai ndio maana akapata woga. Wakati tunakula nikamuona yule bwana kidolechake gumba kimekatwa. Alipokuwa nakata nyama, nikagundua vidole vyake gumba vya mikono vyote vimekatwa. Hapo nilishindwa kujizuia kuwa na shauku, nikataka kumuuliza

kulikoni. Lakini ikabidi nimsubiri amalize kula.

Kumbe wakati ule hata yule mwenye shughuli yake alikuwa anashuhudia yanayotokea. Alikuwa akinisubiri nianza kuuliza. Kwa kuwa yeye ndiye mwenye shughuli isingekuwa vyeka kumkera mgebi wake. Ndipo naye akasubiri amalize kula ili amuulize. Yule bwana alipomaliza kula nikamuuliza “ndugu yangu nimeona hata huugusa chakula hiki “zerbajeh” ama hukupendi” naye akajibu “ninakipenda ila baada ya kula ni lazima nioshe mikono yangu mara 40 kwa maji, mara 40 kwa alita na mara 40 kwa sabuni. Sasa vitu hivi hapa havipo na si vyema kusumbuwa watu kwenye shughuli hii”

Kwa shauku zaidi nikamuuliza ana nini hasa. Ndipo akanieeza kuwa chakula hiki ndio sababu ya yeye kukatwa vidole gumba vya mkono wake. Kisha akatuonyesha na vidole kumba vya miguu yake, pia vimekatwa. Hapo nikapata shauku zaidi kujuwa hasa kwa nini amekatwa vidole gumba vyake vyote vinne kwa sababu ya chakula tu.

Wakati mazungumzo yetu haya yanaendelea yule bwana Mansur mwenye shughuli yake alikuwa anasikiliza. Basi akaagizwa kuletwe ndoo mbili za maji, sabuni na alita. Hapo kopo la kunawia na alita zikaandaliwa kwa ajili ya kutoa povu vyema. Kisha ikaletwa tena sahani yenye zerbajeh. Akaambiwa ale kisha atanawa kama anavyotaka. Basi akala vyema akanywa maji na kumshukuru Mungu. Kisha akaanza kunawa na alita mara 40 kisha sabuni mara 40 kisha maji mara 40. alipomaliza tukamtaka atusimulie hadithi yake ndipo akasimulia hadithi ifuatayo:-

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...

Hadithi ya aliyekatwa vidole gumba

Posti hii inakwenda kukupa muendelezo kuhusu kifo cha mtoa burudani wa sultani

HADITHI YA ALIYEKATWA VIDOLE GUMBA

Mimi nilikuwa mfanyabiashara mdogo sana, katika mji wa Baghdad. Nilikuwa ni muuzaji wa kofia na mikanda pamoja na nguo za ndani za wanawake. Ijapokuwa biashara yangu ilikuwa ni ndogo lakini ilikuwa ikinitosheleza kupata rizki . sikupata kuwa na mke wakati huo. Katika sehemu tulipokuwa tukiuza mimi ndiye niliyekuwaga mgogo pekee, nikiwa na miaka 21, huku sharubu ndio

zilikuwa zikianza kuota.

Siku moja akaja msichana mmoja wa kitajiri sana, niligundua hilo baada ya kumuona amepanda farasi mzuri aliyekuwa na matandiko mazuri yenye mapambo ya kupendeza zaidi. Pia alikuwa ameongozana na wajakazi wawili. Alipokuja alionekana kushangaa sana pindi lipokuwa akitazama upande tulipokuwa tumekaa mimi na mwenzangu. Basi alinagiza wajakazi wake wanunue vitu alivyotaka na walipokamilisha waliondoka, huku akiwa anatuangalia. Sikuweza kuioa sura yake wala kusikia sauti yake. Alikuwa ni mrefu wa wstani mwembamba wa kawaida. Mwenye nywele ndefu. Niligundua hilo baada ya kumuangalia vyema pindi alipogeuka.

Sikuwa na umakini naye maana hata hakuwa mteja wangu. Wiki ilipita hatimaye siku ya jumamosi nikamuona tene, siku hii alikuja kwenye biashara yangu na kuulizia mikanda ya wanawake pamoja na ngua za ndani. Akataka nimchagulie nguo ya ndani inayomuenea vyama. Nilistaajabu sana maana katu sijapata mteja aliyewahi kunieleza maneno haya ya kipuuzi. Lakini pia nilistaajabu sana niliposikia sauti yake. Sauti laini, iliyo na mikwaro, nikajikuta moyo unaenda mbio na joto la mwili wangu linaongezeka. Jasho la kwenye makwapa linaanza kunichuruzika. Kwa hakika sijapatapo kusikia sauti tamu kama hii katika maisha yangu yote.

Nilitamani azungumze nami maneno mengine, nipate kuthaminisha zaidi sauti ya binti huyu. Nilipogundua kuwa si mtu wa maneno mengi nikamuuliza, “unava saizi gani” hakunijibu swali langi, alifikiri zaidi ndipo akanijibu “niangalie kwa ukaribu vizuri utajuwa saizi yangu”. mmmmmhhh haya. Hapo nikapata fursa ya kuthaminisha ngombe kwenye gunia. Nilistaajabu sana baada ya kuona mapigo ya moyo yanaongezeka na jasho la kwapa ninanitoka.

Nikaanza kumchagulia niliyoona inamtosha, nikampatia kisha kimpatia na mkanda. Wakati naendelea kuchaguwa alikuwa akiniangalia sana usoni. Alikuwa amefunika sura yake lakini niligundua kuwa alikuwa ananikonyeza. Sikupata kuiona sura yake, lakini niliamini huenda ni mrmbo kama sauti yake. Nilianza kuvutiwa na mteja wangu. Alipomaliza vitu vyake akaondoka bila hata kujuwa anapokaa.

Niliwaza kuwa pindia akija tena nimuulize maswali kadhaa nipate kujuwa nitamkuta wapi pindi nikimtafuta. Hali haikuwa kama nilivyotaka, muda mrefu ulipita bila hata ya kumuona. Baada ya wiki kama mbili akaja tena siku hii akadai kuwa amesahau pesa hivyo anaomba nimkopee atakweda kuniletea pesa siku nyingine. Kwa kuwa nilishaanza kulewa nikakubali kumkopea.

Alichukuwa karatasi na kuanza kutaja bishaa anazotaka. Nikaenda kumkopea vitu vile nikiwa mimi ndiye dhamana. Ilikuwa ni siku ya kipupwe, nilipokuwa ninarudi ghafla nguo aliyoifunika sura yake (nikabu) ikapeperuka, na hapo nikapata kuona sura iliyobandikwa kwenye paji lake. Nilitamani awe ni sanamu liwe nyumbani kwangu. Nilipata kuvutiwa ghafla na urembo wa binti huyu. Niligundua hakuwa na mkunjo hata mmoja kwenye uso wake. Nilizidi kulewa na kupenda.

Nikamletea bidhaa na nikapata kusikia neno ahsante kutoka kwenye kinywa chake. Niligundua anatabasamu pana na la kuvutia. Matukio yote haya yalitokea kwa muda mchache sana. Alichukuwa bidhaa zile na kutokomea mtaani. Nilishikwa na butwaa na nikasahau kumuuliza ni lini ataleta pesa ya watu. Nilipata kugundua kuwa kumbe unaweza kupenda hata kwa siku moja.. sikuweza kula, kulala wala kusinzia, kana kwamba sira yake ilikuwa ipo ukutani.

Niliamaka usiku nikakamata nguzo na kushika ukuta huku nikiufananisha ndiye yeye. Hatimaye nikapitiwa na usingizi paleplae. Asubuhi nilijikuta nipo chini, nikakumbuka hasa nini kilitokea. Wii moja, mbili na hatimaye mwezi ukapita bila ya kutokea, na huku ninadeni lake. Wenye mali zao walikuwa wakinitaka nilipe pesa yako. Mikawa nawwhidi kuwa nitawalpa kesho.

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

Hadithi iliyoanzia kisimani na kuleta mshangao kati ya mrembo mke wa Mtu na kijana shupavu wa kijijini...